

**Issue no:** 01 | **Vol no:** 06 | **August** 2025: 14-23

# Matumizi ya Umajazi wa Kitashtiti katika Usawiri wa Wahusika na Maudhui: Mfano wa riwaya ya *Utengano*

**Dave Bowen**

**Kabarak University, Kenya.**
Main author email: tbowenza001@gmail.com

**Article History**
Received: **2025.06.01**
Accepted: **2025.07.02**
Published: **2025.08.01**

**Cite this article in APA**
Bowen, D. (2025). Matumizi ya umajazi wa kitashtiti katika usawiri wa wahusika na maudhui: Mfano wa riwaya ya *Utengano*. *Editon consortium journal of kiswahili*, *1*(6), 14–23.
https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v6i1.603

**Ikisiri**
Utafiti huu ulilenga kuhakiki matumizi ya mbinu ya umajazi wa kitashtiti katika kuwasawiri wahusika na kuyaendeleza maudhui katika riwaya ya *Utengano* (Said Ahmed Mohamed). Umajazi ni mbinu muhimu katika utunzi wa kifasihi. Madhumuni ya utafiti yalikuwa kuhakiki namna mbinu ya umajazi wa kitashtiti umetumiwa kuifumba maana maalum katika riwaya teule. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Umuundo. Umuundo unaeleza lugha kama kiungo kamili kinachojisimamia. Lugha ni mfumo wa uhusiano kati ya viungo kadhaa vinavyoijenga. Mathalan maana kamili ya sentensi hutokana na kuunganishwa na kuambatanishwa kwa viungo mbalimbali kama vile nomino, vivumishi, vitenzi na vielezi. Matumizi ya Umuundo katika uhakiki wa fasihi hutuelekeza kuitazama fasihi kama mfumo ambao unajumlisha vipengele kama: fani na maudhui ambavyo huchangia ukamilifu wake. Vipengele hivi huchangiana na kukamilishana katika kazi ya fasihi kama vile riwaya. Ukusanyaji wa data ulifanyika maktabani. Riwaya teule na makala zinazohusiana na mada zilisomwa. Data zilidondolewa, zikachujwa, zikachunguzwa na kisha zikachanganuliwa kwa kutumia utokezi katika riwaya na kupambanua majina ya majazi ya kitashtiti na kuwekwa katika majedwali. Pia, ilibainika kwamba kando na maudhui yanayotokea katika umajazi wa jina na wahusika vile vile wanayakuza maudhui mengine nje ya umajazi wa majina yao. Aidha, utafiti uligundua kwamba mbinu ya umajazi wa kitashtiti una mchango mkubwa katika kuwasawiri wahusika, na kuyakuza maudhui katika riwaya ya *Utengano*. Matokeo ya utafiti huu yatawasaidia wahakiki wa fasihi, waandishi, walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili na hata vyuo kuhakiki matumizi ya majina ya umajazi katika kazi za fasihi kama vile tamthilia, hadithi fupi na riwaya.

**Maneno muhimu**: Maudhui, riwaya, umajazi wa kitashtiti, umuundo, wahusika.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

**UTANGULIZI**

Utafiti huuulilenga kuchanganua matumizi ya mbinu ya umajazi wa kitashtiti katika kuwasawiri wahusika na kuyaendeleza maudhui katika riwaya teule ya *Utengano*. Matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa kwa wanafunzi, walimu, waandishi na wahakiki wa kazi za fasihi katika kubaini umuhimu wa matumizi ya majina ya umajazi wa kitashtiti katika kazi mbalimbali za fasihi, aghalabu katika utanzu wa riwaya. Makala hii, inajumuisha yafuatayo; mapitio ya maandishi kuhusu dhana riwaya na yaliyoandikwa kuhusu mada. Dhana ya majazi imefafanuliwa na yale yaliyoandikwa juu ya mada hii katika vitabu, tasnifu na majarida yameelezwa. Aidha, nadharia ya Umuundo ambayo iliongoza utafiti huu na mihimili yake imefafanuliwa, Pia, matokeo na majadiliano ya utafiti yameshughulukiwa, kisha hitimisho na mapendekezo yamedhihirishwa.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Riwaya ni mojawapo ya tanzu za bunilizi katika fasihi. Huu ni utungo wa kinathari unaosimulia kisa kimoja au visa kadhaa, wenye upana wa kimawanda na kiwakati, uchangamano wa kimtindo na kidhamira na kina cha uhusika kinachohusisha undani wa kisaikolojia na ubainishaji wa misukumo ya kitendaji na wenye urefu wa kiasi fulani (Wamitila, 2008). Kwa mujibu wa Chimera na Njogu (1999), riwaya ni utungo mrefu wa kubuni, na wenye ploti, unaotumia lugha ya nathari. Naye Mbatiah (2016) anasema riwaya ni utungo mrefu wa kubuni ambao ni mwigo wa maisha halisi katika jamii, unaoandikwa kinathari, wenye mwanda mpana wa kimaudhui, wahusika kadhaa wanaokuzwa, picha kamili ya mandhari na msuko changamano. Riwaya ni utanzu wa kipekee kwa sababu mwandishi ana nafasi ya kusawiri wahusika na mandhari kwa kina na pia kuyaendeleza maudhui yake kwa undani akitumia mbinu mbalimbali.

Urefu wa riwaya umezua mjadala. Wahakiki wa Ulaya kama vile Gardener (1959) wanashikilia kwamba kigezo cha idadi ya maneno ni muhimu katika kuainisha utanzu huu au kusuluhisha suala hili la urefu. Wahakiki hawa wanasema kuwa riwaya lazima iwe na idadi ya maneno yasiyopungua 60,000.

Riwaya ya Kiswahili imeingia katika fasihi ya Kiswahili wakati wa ukoloni wa kimagharibi. Riwaya ya Kiswahili ina msingi wake katika ngano za fasihi simulizi, baada ya kuingia wageni wa kimagharibi, hasa wamishenari. Ngano kadha wa kadha zilitafsiriwa na zikawa ndio msingi wa riwaya ya kisasa (Chimera & Njogu, 1999). Baadaye, riwaya za kimagharibi zilitafsiriwa katika Kiswahili. Baadhi ya tafsiri hizo ni: *Mashimo ya Mfalme Suleiman*, *Kisiwa Chenye Hazina*, *Mashujaa* na *Safari ya Guliva*, zilizoandikwa na Rider Haggard, R.L Stevenson, Charles Kingsley na Jonathan Swift mtawalia. Riwaya halisi za kwanza ziliandikwa na Shaaban Robert, alikuwa mwasisi wa riwaya za Kiswahili (Mutembei, 2012). Riwaya za kwanza za Kiswahili zilikuwa *Kusadikika* (Robert, 1951) na *Adili na Nduguze* (Robert, 1952).

Riwaya huwa na vipengele vifuatavyo: Maudhui na fani. Kipengele cha fani hujengwa na wahusika, mandhari, mtindo, ploti na matumizi ya lugha (Wamitila, 2010). Kwa mujibu wa Mutembei (2012), maudhui na fani ni kama jozi za utungo mmoja. Wahusika ni nguzo muhimu katika kukamilisha riwaya kwa kukuza maudhui. Kwa hivyo, maudhui na wahusika ni masuala muhimu yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi, riwaya ikiwemo. Ili riwaya iwe kamilifu, vipengele vyote hivi ni sharti viingiliane. Vipengele vyote vile vile huchangiana na kukamilishana. Kwa hivyo, kipengele cha wahusika ni muhimu katika riwaya. Watunzi huwatumia wahusika wao kupitisha falsafa, dhamira na maudhui yao. Wamitila (2002), anasema wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Wahusika wa kazi za fasihi huwa binadamu, wadudu, wanyama, majini au mazimwi. Mhusika akiwa binadamu, kwa mfano katika riwaya, anaweza kuwa na sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na wanayoyatenda.

Mlacha (1985) anaona wahusika kama watu tunaoishi nao ambao wamechujwa, wamechunguzwa, na kusomwa tabia zao, matendo na sifa zao, halafu wakachukuliwa kama mifano bora ya kuweza kutoa sifa halisi. Mlacha anaendelea kusema kuwa mojawapo ya sifa za usanii mzuri ni uumbaji wa mhusika kulingana na maisha halisi. Uumbaji wa wahusika ni utungaji wa picha ya mawazo ya watu waliobuniwa kwenye hadithi kiasi kwamba msomaji anaweza kuwaona kama watu halisi na wanaoishi katika jamii halisi. Hata hivyo, mtunzi ana uhuru wa kuwapa majina wahusika wake kutegemea malengo yake, kwa mfano anaweza kufumba maana kwa kuwapa wahusika wake majina ya umajazi wa kitashtiti. Kila msanii ana mbinu zake za kuwaumba wahusika wake. Njia mojawapo ya kuwaumba wahusika ni kuwapa majina. Baadhi ya majina ya wahusika yanakuwa majazi

ama yanayoashiria jamii pana ya Afrika Mashariki (Wamitila, 2010; Kavoi, 1996).

Watunzi wengi wa riwaya nyingi za Kiswahili wameendelea kuwatumia wahusika wa aina mbalimbali na wenye majina halisi au majina ya kimajazi. Oriedo (2001) anasisitiza kwamba katika riwaya au kazi yoyote ya fasihi, ni muhimu kuzingatia majina ya wahusika, maingiliano yao na wenzao, tabia na vitendo vyao, wanachosema, kile wahusika wengine wanasema juu yao na hatimaye nafasi walizochukua katika riwaya au kazi yoyote ile ya fasihi. Wahusika huchangia katika uendelezaji wa maudhui katika riwaya. Uteuzi na uumbaji wa wahusika hutegemea nia na lengo la mwandishi. Mtunzi hufanya uamuzi ama awatumie wahusika wenye majina halisi au majina ya kimajazi. Chimerah na Njogu (1999) wameainisha wahusika kwa kutumia vigezo vya sifa, nafasi na tabia zao.

Kwa mujibu wa Msokile (1992), maudhui ni mawazo, fikra na ujumbe uliomo katika kazi ya fasihi. Wamitila (2002) anatoa fasili ya maudhui kama jumla ya masuala na mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Katika kuikuza dhamira yake, mwandishi anayaibua na kugusia maudhui. Wamitila (2003) anasema maudhui ni jumla ya mambo yote yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Aidha, anasema maudhui hutumiwa kwa mapana kujumuisha dhamira, falsafa, itikadi na msimamo wa mtunzi. Maudhui hudhihirishwa katika kazi ya fasihi kupitia wahusika. Wahusika ndio wanayasukuma na wanayahimili maudhui katika kazi ya fasihi (Chimerah & Njogu, 1999). Kwa hivyo, vipengele vya wahusika na maudhui katika tungo za kifasihi vina uhusiano wa karibu sana. Mbinu anazotumia mtunzi katika kuwajenga wahusika kama vile umajazi kwa kiasi kikubwa huathiri uwasilishaji wa maudhui yake.

Wahusika katika kazi za fasihi wanaweza kusawiriwa kwa njia nyingi kutegemea msanii. Wamitila (2010) ameelezea mbinu kadhaa. Kwanza, anasema wahusika wanaweza kusawiriwa kwa mbinu ya kisimulizi ambapo mhusika anasawiriwa kwa usimulizi. Wasifu wake, msukumo wa matendo yake, mazingira yake, tabia na amali zake zinasimuliwa na msimulizi ambaye anataka msomaji aone mtazamo wake. Pili, ni mbinu ya kidrama, ambayo huwaonyesha wahusika wakitenda matendo na kuzungumza. Mbinu hii huwapa wasomaji nafasi ya kuona na kuzichanganua tabia za wahusika bila kuambiwa moja kwa moja kutokana na matendo au mazungumzo yao. Uchanganuzi huo wa wasomaji hauathiriwi na mwandishi au mtunzi kama ilivyo katika matumizi ya mbinu ya kisimulizi.

Tatu ni mbinu ya uzungumzi nafsiya ambayo ni mtindo wa kuyawasilisha mawazo ya mhusika kwa mtindo au njia ya kujizungumzia. Hii ni kinyume na mbinu ya dayalojia inayohusisha mazungumzo baina ya wahusika. Nne, ni mbinu ya kisitiari ambayo ni ulinganishi wa moja kwa moja bila kutumia vifananishi. Badala yake hutumia kitenzi kishirikishi "ni". Mbinu hii inaweza kutumiwa katika usawiri na uendelezaji wa wahusika na hata mandhari. Tano, ni mbinu ya kimajazi. Hii ni mbinu ya kutumia majina ambayo hufumbata sifa ya wahusika na mandhari wanaopatikana katika kazi za kifasihi zinazohusika. Hii ni mbinu ambayo inachukuliwa kumrahisishia msomaji kazi ya kuwaelewa wahusika wanaopatikana katika kazi inayohusika (Wamitila, 2008). Majina haya ya kimajazi huwa mafumbo yanayoashiria maana, kwa mfano, Hasidi, Kazibure, Huzuni, Majivuno au Mashaka.

Si kila mwandishi huyatumia majazi. Majazi ni mbinu ya kutumia majina ambayo hufumbata sifa za mandhari na wahusika wanaopatikana katika kazi ya fasihi (Mbatiah, 2016). Kwa upande mwingine umajazi wa kitashtiti ni mbinu ambayo mwandishi hujenga majina ya wahusika na mandhari kwenye msingi wa kitashtiti (Wamitila, 2010). Mwandishi hutumia mbinu hii kufichua uovu au ujinga uliopo katika jamii. Mwandishi hutumia majazi kwa madhumuni fulani, mathalan majazi yanaweza kutumiwa kufumba maana au kusawiri sifa, tabia na matendo ya mhusika au wahusika kuendeleza maudhui fulani. Kwa mfano katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* (1976), jina la kimajazi Sulubu limetumiwa kwa maana ya mhusika anayepitia shida au dhiki na kazi za sulubu katika maisha yake. Maisha ya mhusika huyu yanaakisi sifa hizi. Huu ni ufundi wa kipekee wa watunzi wa kazi za fasihi.

Shaaban Robert ameyatumia majina mengi ya majazi katika riwaya zake, mathalan katika riwaya ya *Kusadikika* (Robert, 1951) kuna mhusika Majivuno ambaye mtunzi amemsawiri kama mwenye majivuno katika matendo yake yote. Sifa na tabia zake zinalandana na maana ya jina lake. Aidha, katika tamthilia ya *Visiki* (1984) mtunzi amewapa baadhi ya wahusika wake kama vile Matanga na Huzuni majina ya kimajazi. Kama yanavyoashiria majina yao, ni wahusika wenye huzuni na majonzi kutokana na mateso wanayopata. Baada ya kuchochewa wanawaangamiza wengi huku wakizusha

matanga. Wakati mwingine, majina ambayo mwandishi anawapa wahusika na mandhari yake ni majina halisi katika jamii, kwa mfano Yohana, Yusufu, Hamisi, Otieno, Kipkemoi, Mweni, Wanjohi, Bondeni, Mlimani au Majimoto. Mtunzi anafanya uteuzi wa mandhari na wahusika wake kutegemea malengo na mtindo wake.

Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kuhakiki matumizi ya umajazi wa kitashtiti katika kusawiri wahusika na kukuza maudhui katika riwaya Kiswahili ya *Utengano*. Katika mbinu ya majazi mwandishi huyapa wahusika majina kulingana na sifa zao au kufumba maana fulani (Wamitila, 2010). Umajazi wa kitashtiti huchochea msomaji kuyatafakari zaidi kuhusu maudhui yanayoshughulikiwa.

**Misingi ya Kinadharia**

Nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2014). Nadharia ni muhimu katika kuongoza utafiti wowote ule. Nadharia ni muhimu zaidi katika kuhakiki kazi ya fasihi. Nadharia huupa utafiti umadhubuti (Matundura, 2007). Uamuzi wa mtafiti kuhusu suala la fasihi ni sharti litokane na misingi ya nadharia ya fasihi. Buliba et al. (2014) wanasema nadharia hutoa mwongozo wa kutafakari masuala maalum katika utafutaji wa maarifa kwenye taaluma mahususi, fasihi ikiwemo. Kwa hivyo, nadharia ni nguzo au mwongozo mahususi wa kazi ya utafiti na husaidia katika kutoa uamuzi na thibitisho kuhusu kazi ya fasihi. Kwa hivyo utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Umuundo.

Umuundo katika fasihi ni nadharia ambayo ilikuwa tokeo la upanuzi wa nadharia ya lugha ya Ferdinand (1857-1913) kutoka kwa uchunguzi wa sentensi na kuitumia katika nyanja nyingine kama anthropology, utamaduni pamoja na fasihi (Kaplan, 1986; Peck & Coyle, 1984). Umuundo una msingi wake katika Urasimu (Wamitila, 2002; *New Encyclopaedia Britanica*, 2003; Scholes, 1974). Baadhi ya wataalamu waliohusika na Urasimu ni wale waliohusika na kuendeleza nadharia ya Umuundo, baadhi ya wataalamu hao ni: Roman Jakobson, Trubetzkoy, de Courtenay na Rene Wellek.

Uchunguzi zaidi wa Umuundo uliendelea katika miaka ya arobaini. Roman Jakobson alichangia katika kuasisiwa kwa kikundi cha isimu cha New York cha Isimu kilichowahusisha watu kama Claude Levi- Strauss; mwana-anthropolojia ambaye mawazo yake yamekuwa na athari kubwa katika nadharia ya Umuundo. Wahakiki wa Kifaransa wanaohusishwa na Umuundo kwa upande ule mwingine ni Ronald Barthes na Tzevetan Todorov. Wahakiki hawa wanahusishwa na mitazamo ya kisemiotiki na kinaratolojia ambavyo ni vimelea vya Umuundo (Wamitila, 2002).

Mawazo ya mwanaisimu Ferdinand de Saussure yaliiwekea msingi nadharia ya Umuundo. Mawazo yake yalikuwa na athari kubwa katika ukuaji wa nadharia hii (*Encyclopaedia Britanica*, 2003; Wamitila, 2003; Wafula & Njogu, 2007; Carter, 2006). Mwanaisimu huyu alibainisha tofauti kati ya matendo ya kiusemi (*parole*) na mfumo mpana wa lugha (*langue*). Tamko lolote huwa na maana tu ikiwa litaangaliwa katika upana wa msimbo au lugha ya kijumla inayotumiwa na wanajamii. Wafula na Njogu (2007) wanasema Ferdinand alidai kuwa lugha ina sehemu mbili zinazodhihirika katika usemaji:

i) Kuna lugha dhahiri yaani lugha inayojikita katika maongezi ya kila siku.
ii) Kuna lugha dhahania yaani lugha ambayo haibainiki wazi.

Mwanaisimu huyu alisema kuwa lugha ni mfumo wa muundo unaojitosheleza na unaojieleza. Mtazamo wa isimu kama mfumo au muundo unaathiri wahakiki wanaotumia nadharia ya Umuundo kwa kuiona kazi ya fasihi kama mfumo. Wanaumuundo wanashikilia kuwa fasihi imepangwa kama lugha. Lugha ina viwango mbalimbali ambavyo kwa jumla huzaa mfumo wa lugha hiyo (Wamitila, 2003). Matawi mbalimbali ya lugha hayawezi kufasiliwa nje ya muundo huu. Dhima ya kila tawi inatokana na kutegemea kuwepo kwa matawi mengine. Kwa mtazamo huu, wahakiki wa Umuundo waliamini kuwa matini ya kifasihi huwa na mpangilio wa viwango mbalimbali vinavyohusiana na kukamilishana.

Scholes (1974) anashikilia mawazo kwamba ni muhimu kutumia nadharia ya Umuundo katika uhakiki wa fasihi kwa sababu lugha na fasihi zina uhusiano mkubwa sana kwani fasihi hutumia lugha kama nyenzo ya kuyapitisha maudhui ya wasanii. Lugha ni malighafi ya fasihi. Matumizi ya nadharia ya Umuundo katika uhakiki hutuelekeza kuitazama fasihi kama mfumo ambao unajumuisha sehemu kama maudhui na fani. Athari ya asili ya kiisimu bado inajitokeza sana katika uwanja wa fasihi.

Mhakiki wa kimuundo anapaswa kutambua vipengele mbalimbali vinavyoujenga mfumo unaotawala matumizi

ya nadharia ya Umuundo na namna ya kuviunganisha (Jefferson & Robey 1986).

Wafula na Njogu (2007) wanaendelea kusema kuwa namna lugha inavyojipambanua kama mfumo wenye muundo maalum, ndivyo tungo za kifasihi pia zinavyojidhihirisha kama mfumo wenye muundo kamili. Kazi za kifasihi hujengwa na vipengele kama vile maudhui, ploti, wahusika, mandhari, muktadha na lugha. Hakuna kipengele cha fasihi miongoni mwa hivi kitakachoelezwa vizuri katika upekee wake. Lazima kielezwe kwa kuzingatia kuwepo kwa vipengele vingine. Kwa mfano, katika kuwafafanua wahusika katika riwaya teule, ilibidi lugha yao iangaziwe na kushirikishwa. Ni kwa msingi huu ndipo tulichunguza namna mbinu na umajazi wa kitashtiti ilivyotumika kuwasawiri wahusika na kuyakuza maudhui katika riwaya zilizochunguzwa katika utafiti huu.

Nadharia ya Umuundo inashikilia kwamba dunia ni umbo lisiloweza kugawika Scholes (1974). Dunia haikuundwa kwa viungo vinavyoweza kutenganishwa na kujisimamia bali imeundwa kutokana na mahusiano ya miundo. Hii miundo inapaswa kufikiriwa kijumla. Kwa mtazamo huu, kazi ya sanaa hujengwa na kukamilishwa na vipengele vyake mbalimbali. Vipengele hivyo haviwezi kujisimamia bila kutegemea vipengele vingine vya sanaa. Kwa jumla, vipengele vya kazi ya kisanaa kama vile riwaya hutegemeana na kuhusiana katika kuleta maana kamili (Scholes, 1974; Hawkes, 1977).

Nadharia ya Umuundo husisitiza vipengele vya kazi ya sanaa, jinsi vinavyohusiana hadi kuikamilisha kazi ya fasihi. Nadharia hii haiangalii kila kipengele peke yake lakini huangalia mahusiano yaliyoko baina ya vipengele vyote. Vipengele huhusiana kama viunganisho vya mkufu na huamua uhusiano wao (Scholes, 1974). Kila kipengele huwa na jukumu lake maalum. Huangalia namna sehemu mbalimbali za kazi ya sanaa zimefungamana. Kwa mfano, riwaya huangaliwa kama zao linalojitosheleza. Riwaya ina maudhui, ploti, wahusika na mbinu mbalimbali za kusimulia ambazo huingiliana, huchangiana na hukamilishana. Mambo haya hufanya riwaya kuwa muundo unaojitosheleza (Hawkes, 1977). Kutokana na maelezo haya, utafiti huu uliangalia fani ya lugha ya kimajazi ilivyochangia kusawiri wahusika na kukuza maudhui katika riwaya ya *Utengano.*

Nadharia hii ya Umuundo iliangalia lugha kama chombo kinachojitosheleza na haipaswi kufungwa na mikatale ya miktadha na utamaduni. Wanaumuundo waliona ni mwafaka zaidi kuchambua lugha ya mwandishi bila kuzingatia mambo mengine nje ya kazi ya fasihi husika. Kwa ujumla, Umuundo huu unasisitiza kwa kiasi kikubwa fani na kuchunguza kwa undani kazi fulani ya kifasihi (Wamitila, 2003). Wanaumuundo walisisitiza sana ufasihi kwa kuchunguza mbinu mbalimbali za fasihi.

Wahakiki wa Umuundo Mpya wa Amerika wakiongozwa na John Crowe na Cleanth Brooks, pia walisisitiza vipengele vya ndani vya matini ya fasihi na kupuuza wasifu wa mwandishi. Walisisitiza umuhimu wa uhakiki wa kusoma kazi za sanaa kwa ukaribu na kwa undani. Msokile (1993) anasema kazi ya sanaa kwa mkabala huu huangaliwa kama kitu kisichohusiana na jambo jingine nje ya kazi yenyewe. Mhakiki huikabili kazi ya kifasihi kwa kuchunguza vipengele vya kazi hiyo na kuona jinsi vinavyohusiana na kujengana.

Baadhi ya sifa za nadharia hii ya Umuundo ni kama vile kuamini kuwa sanaa inajisimamia yenyewe na kuwa ni chombo kinachojitosheleza. Kwa hivyo, hamna haja kutumia mambo ya nje kuhakiki kazi ya fasihi. Sanaa inafaa ichunguzwe kwa msingi wa sanaa yenyewe. Umuundo humpuuza mwandishi katika uhakiki wake ili kufichua au kuweka wazi mifumo au harakati za kiuashiriaji ambazo zinatokana na kazi hiyo. Umuundo unatilia mkazo miundo ya kiuashiriaji katika kazi ya fasihi. Kazi ya fasihi hasa ushairi inaufanya ulimwengu uonekane tofauti, kupinga hali ya mambo vile yanakuja kwa tajiriba ya kila siku. Mpangilio wa vitushi unaonekana katika hadithi lakini mambo ya kawaida yasiwe ya kawaida.

Katika fasihi, Umuundo unachukulia kuwa usayansi wa fasihi huegemea fani wala si maudhui (Rice & Waugh, 2001). Umuundo huangalia umoja au ushikamano kati ya mfumo wa uandishi na kuangalia matini kama uamilifu wa mfumo wa fasihi na kuutenganisha na historia na muktadha wa kijamii. Kwa hivyo, Umuundo huegemea zaidi fani ya kazi ya sanaa. Hii hujumuisha: mbinu za masimulizi, muundo wa hadithi au ushairi, lugha ilivyotumika kwa mfano msamiati na uteuzi wake, takriri, tashibiha, istiari na kejeli.

Kwa mujibu wa Saussure, chombo asili cha isimu ni mfumo wa lugha tu (*la Langue*). Mfumo wa lugha ni

muundo unaodhaniwa si kihistoria tu bali pia katika jamii ulimotungiwa na mchakato wa kisaikolojia unaopatikana na kutumiwa katika tabia ya lugha. Saussure anashikilia kuwa kila mfumo wa lugha una upekee na kwa hivyo uelezwe katika miktadha yake. Anachukulia kuwa kile kinachoashiriwa kina uhusiano wa kinasibu na kiashiria chenyewe (Lyons, 1981; Yule, 1996, Fromkin na Rodman, 1988). Maana lazima iingiliane na muundo wa lugha. Uhusiano wa kile kinachoashiriwa na maana ni wa kisemantiki wala si wa umbo katika mfumo wa lugha. Ndiyo maana neno moja lile lile linaweza kuwa na maana tofauti katika mifumo miwili ya lugha. Maana ya neno huwekwa na ule mfumo wa lugha. Katika kufafanua uhusiano kati ya kiashiria na kiashiriwa, lazima tuelewe namna ambavyo lugha hutekeleza wajibu wake na vile viashiria hivyo vinavyohusiana na kuungana na wala si kuvitazama viashiria hivyo kila kimoja kivyake. Kwa hivyo, kwa mujibu wa maoni hayo, utafiti huu uliangalia uhusiano uliopo kati ya fani na maudhui katika fasihi kwa kuangazia namna mbinu ya umajazi wa kitashtiti inatumiwa na mtunzi kusawiri wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Utengano*.

Wanamiundo huangalia lugha kama ilivyo katika maandishi yaliyopo. Hawataki kuangalia vile miundo ya maandishi ilivyobadilika kadri ya muda uendavyo (Lyons, 1981). Baada ya kuipitia mihimili ya nadharia ya Umuundo kwa mujibu wa utafiti wetu ilidhihirika kwamba baadhi ya mihimili haiwezi kufaa katika uhakiki wa kazi za kifasihi zenye mwelekeo wa kimuktadha au unaozingatia nafasi ya msomaji na mtunzi wa kazi husika. Hata hivyo, baadhi ya mihimili ni muhimu na ndiyo maana utafiti huu uliteua nadharia hii kama nguzo ya kutafitia suala la utafiti. Kwa msingi huu wa kinadharia, utafiti huu ulizingatia baadhi ya mihimili ya Umuundo. Mihimili mikuu ya nadharia ya Umuundo katika utafiti huu ni kama ifuatayo:

i) Nadharia ya Umuundo huangalia kazi ya sanaa kama zao linalojitosheleza. Husisitiza vipengele vya kazi ya sanaa vinavyohusiana na kufungamana hadi kuikamilisha kazi hiyo. Kila kipengele huwa na jukumu lake maalum. Mhimili huu ulifaa kwa kuangalia namna kipengele cha wahusika kinavyosaidia kuendeleza maudhui katika riwaya teule.

ii) Umuundo husisitiza fani ya kazi ya sanaa. Hii hujumuisha mbinu za masimulizi, muundo wa hadithi au ushairi, lugha ilivyotumika mfano msamiati na uteuzi wake, majazi, takiriri, tashibiha, istiari n.k.

iii) Kama ambavyo lugha ni mfumo wenye muundo maalum, fasihi ambayo hutumia lugha kama malighafi yake ni mfumo wenye vipengele vinavyotegemeana na vinavyoelezwa katika muktadha wa vipengele vingine. Hakuna kipengele cha fasihi kati ya hivyo kitakachoelezwa vizuri katika upekee wake. Kwa hivyo katika utafiti huu, tuliangazia matumizi ya mbinu ya umajazi wa kitashtiti katika kukuza wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Utengano*.

iv) Sanaa inajisimamia yenyewe na ni chombo kinachojitosheleza, kisichobadilika na kuwa inaendelea. Kwa hivyo hamna haja kutumia mambo ya nje kuhakiki kazi ya fasihi. Sanaa yafaa ichunguzwe kwa msingi wa sanaa yenyewe. Mtazamo huu ni kuchunguza kwa undani kazi ya fasihi. Katika utafiti huu data za kimsingi zinatokana na uchanganuzi wa matini ya riwaya ya *Utengano*.

Kwa kuegemea mihimili hiyo mahususi utafiti huu ulihakiki matumizi ya mbinu ya umajazi wa kitashtiti katika kusawiri wahusika na kukuza maudhui katika riwaya ya *Utengano*.

## MATOKEO NA MAJADILIANO YA UTAFITI

### Riwaya ya Utengano

*Utengano* ni riwaya inayozunguka familia ya mhusika mkuu Maksuudi. Mtunzi anaangazia suala zima la ndoa na malezi na madhara yake. Mhusika Maksuudi ana familia yake, Tamima, mke wake na watoto watatu: Mussa, Maimuna na mtoto wa kiume aliyezaliwa. Maksuudi ni tajiri anayejipatia mali kupitia unyakuzi baada ya wakoloni kuondoka. Ana tamaa ya mali na ni fisadi. Pia ni mnafiki anayeonyesha kwamba yeye ni Mwisilamu halisi lakini ni asherati. Ana kimada kwa jina Kazija ambaye anaandamwa pia na Mussa mwanawe Maksuudi. Kwa hivyo, Makusuudi ni mnafiki. Anajificha katika dini kutenda maovu.

Maksuudi ana hasira kama mkizi. Anaongoza familia yake kiimla. Ni mkali na anawaweka wanawake nyumbani na kuwanyima ruhusa ya kutoka nje. Hapo awali alikuwa amemtesa binti wa Farashuu hadi akafa. Ukatili wake pia unaonekana pale anapomkuta Mussa

kwa Kazija na kumchapa nusura amuue. Aidha, anamtandika Tamima anapong'amua amejifungua na kumruhusu mkunga kuingia kwake. Hasira zake zinazidi anapogundua kwamba Maimuna hayumo nyumbani usiku huo.

Mtunzi vile vile anazidi kuonyesha kuwa matendo mabaya ya mtu humfuata na yana madhara yake. Kwa mfano, Maksuudi, kutokana na maisha yake ya uasherati, unafiki, ukatili, ufisadi na tamaa, anaishia kufungwa na kupoteza familia yake. Watoto wanamtoroka na bibi anamwacha hali inayomsababishia Maksuudi shida chungu nzima. Maksuudi anadhoofika kiafya na hatimaye anajuta na kuungama makosa yake.

Aidha, ni dhahiri kwamba mwisho wa kosa, kunayo matumaini na nafasi nyingine ya mtu kujikosoa. Mtunzi anaonyesha Maksuudi akijutia maisha na matendo yake baada ya kuona mabadiliko yanayotokea katika maisha yake. Akataka asamehewe na wote aliowakosea. Maimuna pia, baada ya kutoroka nyumbani akiwania kupata uhuru wa maisha yake, anajikuta amejiingiza katika maisha ya ulevi na ukahaba. Anakuja, kujuta na kubadilika na kuanza maisha mapya.

Kwa ujumla mwandishi anaonyesha utengano mwingi miongoni mwa wahusika mathalan Maksuudi anatengana na ndugu yake Inspekta Fadhili, watoto wake Maimuna na Mussa, wakeze Tamima Bintiye Farashuu, Farashuu wananchi na kadhalika. Ulipizaji wa kisasi pia unaangaziwa na mtunzi. Farashuu, Kazija na Biti Kocho wanapanga njama ya kulipiza kisasi kwa Maksuudi na wanaapa kusambaratisha familia yake. Lengo lao lilianza kufanikiwa baada ya Maimuna kutoroshwa nyumbani.

Kwa ujumla mtunzi anashughulikia maudhui makuu kama vile kisasi, majuto, ndoa, uzazi, ufisadi na unafiki. Mtunzi kwa kweli amefanikiwa kumtumia Maksuudi kuonyesha namna tamaa ya uhuru na uongozi unavyowavunja moyo wananchi. Matarajio ya wananchi baada ya uhuru hayakutimizwa kwa sababu ya tamaa, ufisadi na udanganyifu wa watu kama kina Maksuudi.

**Majina ya umajazi wa kitashtiti katika riwaya ya Utengano**

Mtunzi Mohamed Saidi ameyatumia majina ya umajazi wa kitashtiti katika riwaya yake ya *Utengano*. Majina haya yanajitokeza wazi na kudhihirisha umajazi huo. Vile vile majina haya yametumika kukuza maudhui mbalimbali. Uchanganuzi wangu, ulidhihirisha madhari na wahusika wafuatao kama wahusika wenye majina ya umajazi wa kitashtiti: Shoka, Inspekta Fadhili, Liwazoni na Pumziko. Aidha, mtunzi ameyatumia majina ya umajazi wa kitashtiti katika riwaya kuyakuza maudhui kama vile: Unafiki, mabadiliko na ukahaba.

**Shoka**

Shoka ni kifaa kizito cha chuma chenye makali na kilichotiwa mpini aghalabu wa mti na kinachotumika kwa kutema au kuchanja kuni, miti, na migogo (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2014).

Shoka kwa kawaida ni kifaa kinachotumiwa kuchanja kuni, na kama ni silaha. Si silaha hatari na yenye makali. Hukata magogo kushinda upanga. Mtu anayepewa jina hili la Shoka anatarajiwa kumiliki sifa za shoka kama vile ukali, uhodari, nguvu, kiongozi, uwezo na mwenye kuhimidi maswala mazito. Mhusika Shoka anadhihirisha kinyume cha ubabe, kuhimili shida, uhodari, ukali na nguvu. Wanawake wanamdunisha kwa sababu nguvu zake zote zimeliwa na ulevi wake. Shoka anapuuzwa na kukaripiwa na wanawake kwa sababu yeye amekosa uhodari, heshima na hadhi. Kwa hivyo Said anamsuta Shoka kwa kumsawiri yeye kama mwanamume aliyekosa nguvu na ubabe katika maisha yake. Mtunzi kwa hali hii, anamcheka na kumsuta mtu huyu kuwa ni 'Shoka butu' kwa wanawake kwa sababu ya ulevi. Tabia hii haifai kwa mwanamume yeyote yule.

Aidha, Mwanamume anatarajiwa kuwa na udhibiti na mwelekeo katika maisha. Hata hivyo, Shoka katika jumuiya ya riwaya ya *Utengano* anafanya na kudhihirisha kinyume cha jina lake. Hamiliki sifa zozote za shoka. Kwa familia yake amefeli. Hakidhi mahitaji ya mke wake na wanawe. Selume mkewe amechoshwa na udhia wake mtunzi anasema:

> "…Naam, Selume amechezwa na mwanamme huyu. Ametwishwa mzigo mzito
> Asioweza kuubeba. Si mchezo kwake kujaza chungu cha kumtosha yeye na watoto wake na huyo Shoka, ambaye haleti chochote kwake lakini hodari wa kungoja kimeshapikwa apande." (uk 110).

Dondoo hili linadhihirisha uzembe wa Shoka katika wajibu wake kama mume na baba. Shoka si mwanamme. Shoka ni ajizi na haleti chochote nyumbani. Mtunzi anamsawiri Shoka kama mhusika asiye na sifa za mwanamume. Amepoteza hadhi yake katika jamii.

Aidha, Shoka ni mlevi na hawezi chochote. Maimuna hata anamkejeli kwa kusema :

> "… wewe unayejua ungalikuwa hivyo, Shoka? Shoka gani huchanji kuni wala hukati magogo.." (uk 113)

Vile vile, Kijakazi anamkejeli Shoka:

> " Shoka Shoka, Shoka gani nalo la kuchanja kuni? Unayetoka roho ni wewe..."(uk 142).

Maelezo hayo kutoka wahusika wawili wa kike, yanaonyesha kuwa Shoka ni 'shoka butu' lisiloweza kufanya chochote na hastahili kumiliki jina hilo. Mwandishi ametumia umajazi wa kitashtiti kukejeli wanaume ambao wanajigamba kuwa wao ni dume lakini hawezi kutekeleza haja za ngono. Wanaishia kuwa watu wasio na thamani yoyote kama shoka butu lisilochanja kuni au hata kutekeleza kazi yake vilivyo.

Mtunzi ametumia umajazi wa kitashtiti wa Shoka kuufichua udhaifu wa mwanamume katika jamii. Umbo la kiume halitoshi tu kudhihirisha sifa halisi za kiume, bali kilichoko muhimu ni matendo na sifa za kiume zinazodhihirishwa kupitia kwa vitendo kama vile ngono na uwezo wa kupata watoto, kuwa na maadili, meko, kujiheshimu, kukidhi mahitaji ya familia yake. Ulevi haujengi mtu na si jambo la kujivunia katika maisha. Aidha, kuwa mume na kuitwa baba hakutoshi, vitendo vizuri vitadhihirisha vilivyo sifa za kiume.

Shoka ni mojawapo wa baadhi ya wanaume ambao wanayakuza maudhui ya kutowajibika maishani. Shoka ni maskini na hana mbele wala nyuma lakini anashinda kilabuni pa Biti Sururu. Shoka ameongeza umaskini uraibu wa ulevi. Shoka anaacha mke wake Salume na kuhangaika akiwafuata uraibu wake wa pombe. Mtunzi anaelekea kutuonyesha kuhusu madhara ya ulevi katika jamii na familia. Maisha haya ya ulevi yanamfanya Shoka kushindwa kukidhi mahitaji ya mke wake Salume na familia yake kwa jumla. Maisha hayo mabaya ya Shoka yalisababisha mkewe Selume kutamauka na kukosa imani katika maisha ya ndoa. Selume anasema kwa ghadhabu:

> "…utumwa, unyonge na manyanyaso ya mwanamume…tupo taabuni wanawake. Huu utumwa kamili…" (uk 112).

Kwa kurejelea nukuu hii, Selume anadhihirisha kwamba amefika mwisho wa hamaki zake kuhusu maisha duni ya Shoka. Mume ambaye hakidhi na kuhudumia familia yake hana nafasi katika jamii. Selume analalamika kila kukicha kwamba hakuwa na mwanamume kutokana na sifa zake Shoka ambazo anamiliki kutokana na ulevi wake. Mtunzi anadhihirisha kwamba mume anayestahili jina la 'mume' anafaa kuhudumia jamaa zake bila kutetereka. Mtunzi amemtumia Shoka kuyakuza maudhui ya ulevi, kutowajibika maishani na umaskini.

**Inspekta Fadhili**

Fadhili kwa mujibu wa *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2016) ni kutoa msaada wakati wa haja au shida; fanya hisani; tajamali au fanya wema. Inspekta Fadhili ni mhusika mkakamavu na mwenye msimamo thabiti. Hatetereki katika kazi yake. Kutokana na jina lake la kimajazi, tungemtarajia awe mtu mkarimu, mcheshi, mtu mwenye wingi wa fadhila na msaidizi lakini kinyume cha hayo, mhusika huyu Inspekta Fadhili ana sifa za kumnyima fadhila zake ndugu yake, Maksuudi. Tungemtarajia Inspekta Fadhili kumhurumia na kumwonyesha fadhila zake Maksuudi lakini anamnyima kwa kumtia mbaroni. Yeye alielewa vizuri mipaka ya ufadhili wake na hakutaka kuvunja sheria za nchi. Aidha, hakuunga mkono ufisadi. Jambo ambalo Maksuudi analiona kama si la kawaida. Maksuudi analalamikia msimamo wa Inspekta Fadhili:

> "…Fadhili anajifanya mzalendo sana. Anasahau hata kwamba damu ni nzito kuliko maji.." (uk 73).

Maksuudi, anatarajia ndugu yake, Inspekta Fadhili, amwauni na amsaidie kama ndugu katika kazi yake ya magendo lakini Inspekta Fadhili anakataa kwani amejitwika jukumu la kuyaimarisha mapinduzi. Inspekta Fadhili ameweka maslahi ya umma mbele ya udugu (Njogu, 1997). Maksuudi angetaka asaidiwe na inspekta Fadhili kusudi ajinufaishe binafsi ilhali Inspekta Fadhili yuko mbioni kuzuia mambo yoyote ambayo yangerudisha nyuma jamii baada ya kupata uhuru.

Aidha, Maksuudi alitarajia Inspekta Fadhili amfadhili na kumsaidia wakati wa shida kwa sababu ya udugu wao. Lakini mhusika Inspekta Fadhili anakataa katakata na kwa hivyo kuonyesha kinyume cha sifa za jina lake la umajazi. Mwandishi ametumia jina Fadhili kama umajazi wa kitashtiti kwa kuonyesha Inspekta Fadhili hafadhili mvunja sheria. Inspekta fadhili anafanya kinyume cha

jina lake. Inspekta Fadhili anakataa kumfadhili ndugu yake Maksuudi na kusema:

> "..mimi Fadhili., mtumishi wa serikali, mtumishi wa umma, niliyeaminiwa kulinda uhuru, haki na usalama wa nchi, hii, niungane na wewe katika kuvunja sheria. Niididimiza kesi, ifutwe, ili wewe ushinde kura…" (uk 75).

Dondoo hili linadhihirisha kwamba Inspekta Fadhili ameamua kutomfadhili ndugu Maksuudi ndugu yake. Msimamo wake ni kinyume cha jina lake. Kutokana na msimamo huo, Maksuudi anakosa ufadhili kutoka kwa Inspekta Fadhili. Mwishowe Inspekta Fadhili hakuhofia wala kusita kumshika nduguye Maksuudi na kumtia mbaroni kwa kosa la jinai badala ya kumsaidia. Kinyume cha matarajio yetu na ishara ya jina lake. Mtunzi anatueleza kwamba ufadhili haramu na unaovunja sheria si ufadhili halisi na halali.

Inspekta Fadhili anajua fika kuwa Maksuudi angeishia kufungwa jela lakini aliamua kutekeleza wajibu wake kama afisa wa polisi. Inspekta Fadhili angemfadhili Maksuudi kwa mikasa yake ya jinai na magendo. Kupitia kwa mhusika huyu mwandishi amedhihirisha kuwa sifa za jina zinaweza kuwa kinyume panapobidi, aghalabu kwa kutenda haki au wajibu kwa mujibu wa sheria za nchi. Kwa hivyo jina la Fadhili limetumika kitashtiti. Mtunzi amemtumia Inspekta Fadhili kuyakuza maudhui ya utengano na uzalendo. Inspekta Fadhili anatetea na kulinda sheria za nchi yake. Aidha, amejitolea kupigana na ufisadi na maovu katika jamii yake. Kwa mfano, anamnyima nduguye, Maksuudi ufadhili wake kwa sababu ya tamaa na mienendo yake mbaya. Anachukia maisha ya ufisadi na unafiki. Hataki kuvunja sheria.

Inadhihirika kuwa mtunzi amewatumia wahusika wenye umajazi wa kitashtiti kuyakuza maudhui katika riwaya yake. Majina yao yanajumuisha majina ya wahusika. Mtunzi amewatumia wahusika wawili, Inspekta Fadhili na Shoka kuyakuza maudhui yake. Kwa mfano, Inspekta Fadhili ametumiwa na mtunzi kuyakuza maudhui ya utengano na uzalendo, huku Shoka ametumiwa kuyakuza maudhui ya ulevi, umaskini na kutowajibika maishani. Kwa hivyo, kuna uhusiano mkubwa kati ya vipengele vya maudhui na wahusika. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, kazi ya sanaa ni zao linalojitosheleza na vipengele vyake vyote vinahusiana na kutangamana ili kazi iwe kamilifu. Kila kipengele huwa na jukumu lake. Katika riwaya ya *Utengano*, mtunzi ametumia wahusika wenye majina ya umajazi wa kitashtiti kuyafanikisha maudhui.

**Jedwali 1: Wahusika wenye majina ya umajazi wa kitashtiti na maudhui wanayoyakuza katika riwaya ya *Utengano*.**

| RIWAYA | MAUDHUI | WAHUSIKA WANAOYAKUZA |
|---|---|---|
| ***Utengano*** | **Utengano** | **Inspekta Fadhili** |
| | **Kutowajibika maishani** | **Shoka** |
| | **Ulevi** | **Shoka** |
| | **Umaskini** | **Shoka** |
| | **Uzalendo** | **Inspekta Fadhili** |

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho:** Katika utafiti huu, niligundua mambo kadhaa kuhusu umajazi kama nyenzo ya kusawiri wahusik na kukuza maudhui. Kwanza, imebainika kwamba mwandishi ya *Utengano* ametumia mbinu ya umajazi wa kitashtiti kusawiri wahusika na kukuza maudhui yao. Aidha, imethibitishwa kuwa kuna ufumbaji wa maana maalum katika matumizi ya umajazi wa kitashtiti katika *Utengano*, mtunzi amesawiri wahusika wenye majina ya umajazi wa kitashtiti kuufumba ujumbe wao. Pia, imedhihirika kutokana na riwaya teule kwamba riwaya ni kazi ya sanaa inayojitosheleza kama inavyojitokeza kwenye mhimili wa nne wa nadharia ya Umuundo na ina vipengele vya fani na maudhui ambavyo huingiliana na kukamilishana, kwa mfano, kipengele cha wahusika husaidia kukuza maudhui katika riwaya.

**Mapendekezo:** Kutokana na matokeo ya utafiti huu ninapendekeza yafuatayo: Kwa vile utafiti huu uliangazia utanzu wa riwaya ya Kiswahili,unapendekezwa utafiti mwingine ufanywe kwa kuangazia matumizi ya umajazi wa kitashtiti katika tanzu nyingine za fasihi kama vile,

Hadithi fupi, Ushairi, Tamthilia, Novela au Fasihi Simulizi. Aidha, katika utafiti huu nililenga matumizi ya umajazi wa kitashtiti katika riwaya ya Kiswahili ya *Utengano* pekee. Kwa hivyo basi, ninapendekeza utafiti mwingine ufanywe kwa kuteua riwaya nyingine tofauti za Kiswahili.

**MAREJELEO**


Buliba, A., Gwachi, G., & Matinde, R. (2014). *Misingi ya nadharia na mbinu za utafiti*. Serengeti Educational Publishers Ltd.

Carter, D. (2006). *Literary theory*. Cox & Wyman.

Chimera, R., & Njogu, K. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Encyclopaedia Britannica, Inc. (2003). *Encyclopaedia Britannica 2003* [Electronic resource]. Encyclopaedia Britannica.

Fromkin, V., & Rodman, R. (1988). *An introduction to language*. Holt, Rinehart and Winston.

Gardener, H. (1959). *The business of criticism*. Oxford University Press.

Hawkes, T. (1977). *Structuring and semiotics*. Methuen.

Jefferson, A., & Robey, D. (1986). *Modern literary theory*. Batsford.

Kaplan, C. (1986). *Criticism: The major statements*. St. Martin's Press.

Kavoi, M. (1996). *Muwala wa vipengele vya fani: Uhakiki wa kazi za S.A Mohamed* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton, Haijachapishwa).

Lyons, J. (1981). *Introduction to theoretical linguistics*. Cambridge University Press.

Mbatiah, M. (2016). *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na maendeleo yake*. Jomo Kenyatta Foundation.

Mlacha, S. (1985). Wahusika katika riwaya za Kiswahili. *Jarida la Mulika*, *17*, Dar-es-Salaam: TUKI.

Mohamed, S. (1980). *Utengano*. Oxford University Press.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya hadithi fupi*. University Press.

Mutembei, A. (2012). *Korasi katika fasihi: Nadharia mpya ya fasihi*. Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili.

Oriedo, H. (2001). *Fani katika riwaya za Shaban Robert: Kusadikika, Utubora Mkulima na Siku ya Watenzi Wote (Uhakiki wa Kiurasmikanuni)* (Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Moi).

Peck, J., & Coyle, M. (1984). *Literary terms and criticism*. Macmillan Educational Books.

Scholes, R. (1974). *Structuralism: An introduction*. Yale University Press.

Wafula, R., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya fasihi istilahi na nadharia*. Focus Books Publishers.

Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya fasihi 1: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Vide-Muwa Publishers.

Wamitila, K. (2010). *Kanzi ya fasihi 1: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Vide-Muwa Publishers.

Waugh, P. (2001). *Modern literary theory*. Arnold.

Yule, G. (1996). *The study of language*. Cambridge University Press.